**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

Mkuu wa Shule 0756042439/0623307579
Makamu Mkuu wa Shule 0694020991
Mtaaluma 0783208812

Shule ya Sekondari Robanda
S. L. P 77
83 Nyamara HM
**31623 Ikoma – Serengeti**
Tarehe 13.05.2026

Ndugu: **…………………………………………….**
Mzazi/ Mlezi wa: **…………………………………**
S. L. P **………………**

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ROBANDA MWAKA …………..**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ……………………………………….amechaguliwa kujiunga na masomo ya Kidato cha **TANO** Tahasusi ya **PCB/CBG** katika shule ya sekondari ROBANDA ambapo atapata Elimu na hatimaye kulitumikia Taifa. Kama Mzazi/Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kulifikia lengo hili la Kitaifa. Aidha, aelewe kuwa ni miongoni mwa Watanzania wachache waliopata nafasi hii adhimu na anapaswa kuitumia vyema.

Shule ya Sekondari Robanda iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara, umbali wa Kilomita 44 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya - Mugumu. Usafiri wa barabarani ni wa uhakika muda wote.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ………….. Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………. Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 Jioni siku za kazi Tu**. Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni si zaidi ya **wiki mbili (siku 14)** tangu tarehe ya muhula wa kwanza kuanza. Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya mapokezi na Usajili.**

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i. Mahitaji yote yaliyoelekezwa katika fomu hii
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

**GEORGE N. CYPRIAN**
**MKUU WA SHULE**

## JINSI YA KUFIKA SHULENI

**i.** Kwa wanaotokea Dar Es Salaam, Pwani, Morogoro, Mikoa ya Kati, Kusini, Nyanda za juu Kusini, Kigoma na Kagera; baada ya kufika Mwanza wanashauriwa kupanda mabasi stendi ya NYAMHONGORO-MWANZA yanayoelekea MUGUMU kupitia BUNDA. Nauli kutoka MWANZA hadi MUGUMU ni kati ya Tsh. 15,000/= hadi Tsh. 16,000/=.

**ii.** Kwa wale wanaotokea Mikoa ya Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga) wapande mabasi yanayokwenda MUSOMA au TARIME kupitia barabara ya NGORONGORO – SERENGETI. Nauli kutoka ARUSHA Mjini hadi ROBANDA ni Tsh. 50,000/= (Kutoka Arusha hadi Kijiji cha Robanda) shukia Kijiji cha Robanda na chukua usafiri wa Boda boda hadi Shuleni kwa gharama ya Tsh 2,000/=

**iii.** Kwa wale wanaotoka Mkoa wa MARA (Musoma MC, Musoma DC, Tarime, Ryorya, Bunda Mji, Bunda V na Butiama) wanaweza kupandia magari kutoka katika Stendi kuu za Mabasi zilizoko maeneo yao kuelekea MUGUMU kupitia Bunda, Musoma, Tarime au Butiama na Kushukia MUGUMU kisha nenda Sheli ya River Oil ambapo utapata magari ya Kwenda Robanda kwa nauli ya Tsh 6,000/= ambapo utashukia senta na kuchukua usafiri wa Bodaboda ambayo ni Tsh 2,000/=

**MAELEZO MUHIMU**

**Kwa siku za hivi karibuni, kumekuwa na utapeli na wizi kwa njia ya Mtandao. Kwa baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kuwa ni Walimu na kuwafahamisha kuwa Mtoto wa Mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni Mgonjwa na yupo Mahututi hivyo mzazi/ Mlezi atume fedha. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi au mtoto wako USITUME CHOCHOTE ni vyema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo**

Mkuu wa Shule 0756042439/0623307579
Makamu Mkuu wa Shule 0694020991
Mwalimu Mlezi wa Bweni (Matron) 0627023046

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

**MAAGIZO NA MAHITAJI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ROBANDA, KIDATO CHA TANO ……….**

**1.0 SARE YA SHULE**.

i. Sketi mbili rangi ya **Karoti** Mashono marinda 3 pembeni ubavu ,rinda moja kubwa mbele na nyuma iwe ndefu ya kufika kifundo cha mguu. Kitambaa cha Karoti kiwe Gredi namba 1 kizito.
ii. Shati mbili **nyeupe aina ya tomato** mikono Mirefu na yenye mfuko Mmoja tu kushoto
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na Kisigino kifupi na Sehemu zote za chini za mguu.
iv. Soksi jozi mbili za rangi nyeupe na ziwe ndefu.
v. Sweta la rangi ya kijivu yenye muundo wa "V" kifuani isiyo na Maandishi wala mchoro wowote.
vi. Kwa wanafunzi wa kiisilam **Hijabu** zao ziwe **nyeupe. Au nusu kanzu (Gauni fupi) ya rangi ya kijivu**
vii. Tai yenye rangi ya karotii yenye michirizi au ufito meupe.
viii. T-Shirt ya Rangi ya **kijivu** yenye kola nyeusi inayovaliwa wakati wa kazi na muda wa jioni hapa shuleni.
ix. T-Shirt ya Rangi ya **Nyeusi plain yenye Kola** ambayo inavaliwa wakati wa darasani siku ya Jumatano.
x. Gauni la kushindia, kitambaa Kizito rangi ya Ugoro. Mshono wa Solo na liwe refu kufika kifundo cha mguu

**1.1 SARE ZA MICHEZO AMBAZO ZITAVALIWA SIKU ZA MICHEZO KWA WANAFUNZI**

Wanafunzi watatakiwa kuwa na nguo kwa ajili ya michezo mbalimbali hapa Shuleni. Hivyo ni lazima kila mwanafunzi aje na nguo hizo kama ifuatavyo:

i. Truck Suit ya Rangi ya **blue bahari** yenye michirizi myeupe.
ii. Viatu vya Michezo (Raba)
iii. T shirt ya michezo rangi ya Blue bahari
iv. Sketi ya kushindia kitambaa cha **kunguru** Mashono marinda 3 pembeni ubavu ,rinda moja kubwa mbele na nyuma iwe ndefu ya kufika kifundo cha mguu kitambaa kiwe Gredi namba 1 kizito. (Kimeambatanishwa hapa)

**Nguo hizi ni za lazima kwa kila mwanafunzi.**

**2.0 VIFAA VYA DARASANI NA MAHITAJI MENGINE YA SHULE**

Mwanafunzi awapo shuleni atasoma masomo yafuatayo:

i. Academic Communication
ii. Geography
iii. Physics (Fizikia)
iv. Chemistry (Kemia)
v. Biology (Baiolojia)
vi. Basic Applied Mathematics (BAM)
vii. Historia ya Tanzania na Maadili

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

Hivyo ni Muhimu Mwanafunzi aje na Vifaa vifuatavyo:

a. Madaftari (QUIRE 3 au 4 pc 11)
b. Dissecting Kit kwa ajili ya somo la Biology
c. Scientific Calculator
d. Lab Coat 1 kwa ajili ya kazi za maabara
e. Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa)
f. Madaftari madogo ya Msomi 10 kwa ajili ya mazoezi ya darasani
g. Rula yenye urefu wa sentimita 30, penseli 3, na kalamu za kutosha
h. Spring File moja kwa ajili ya kutunzia karatasi zake za mitihani mbalimbali
i. Ream **DOUBLE A (2)** kwa ajili ya Majaribio na Mitihani hapa Shuleni. (Kwa mwaka)
j. Begi la kutunzia vifaa vya darasani.
k. Godoro la Sponge upana wa ft 2½
l. Mashuka jozi 2 rangi ya Bluu, Blanketi, Chandarua 1, mto 1, taulo
m. Nguo za ndani za kutosha, ndala/ kandambili za kuogea
n. Ndoo 2 ndogo lita kumi zenye mfuniko; dumu la lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
o. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mfagio ndani (soft bloom)1 na nje 1, mopa 1, dawa ya chooni ya spark kleen 1
p. Sanduku la Bati 1 kwa ajili ya kutunzia vitu vyake (Ni lazima). **Mabegi na masanduku ya thamani kubwa hayatakiwi kabisa shuleni.**
q. Fedha ya matumizi yake binafsi isiyopungua Tsh 40,000/=

### 2.1 MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**NB**: Fedha iwekwe akaunti ya Shule A/C NO 30210008212 ROBANDA SECONDARY SCHOOL RECC A/C na mwanafunzi afike na Bank Pay Slip yenye jina lake ili kurahisisha kazi ya uhasibu. **MWANAFUNZI ASIJE NA FEDHA TASLIMU MKONONI SIKU YA KURIPOTI**

### 2.2 BIMA YA AFYA

Kila mwanafunzi kwa kujali afya yake anapaswa kuja na kadi ya bima ya afya iliyo hai. Hivyo kila mwanafunzi aje nayo kwa matumizi ya afya yake binafsi. Shule haitahusika kumhudumia mwanafunzi asiye na Bima jambo litakalomlazimu mwanafunzi kurudi nyumbani kutibiwa na mzazi atalazimika kutumia gharama kubwa kwa kutuma pesa ya matibabu. Kwa wanafunzi wasiokuwa na Bima wanashauriwa kuja na Tsh 30,000 kwa ajili ya kukata Bima ya iCHF (Bima ya jamii)

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule ya Sekondari Robanda inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu hapa Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni Pamoja na:

A. Heshima kwa viongozi,Walimu, Wazazi, Wafanyakazi wasio Walimu, wanafunzi wengine, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
B. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje kulinganana taratibu za Shule ni lazima.
C. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa na uongozi wa Shule.
D. Kufafanua mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ya na nje ya mipaka hiyo wakati wowote.
E. Kutunza usafi wa Mwili,Mavazi na Mazingira ya Shule.
F. Kuvaa Sare za Shule wakati wote ukiwa shuleni na unapotoka nje ya Shule.
G. Kutunza Mali ya Umma
H. Kutoka nje ya Shule kwa utaratibu maalum yaani ruhusa utakayopewa na Uongozi wa Shule.
I. Kuvaa sare ya shule wakati wote
J. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali bila idhini ya Daktari.
K. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwingine kubadili dini wawapo shuleni.

## 4. 0 MAMBO YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

1. Wizi wa mali ya shule na wanafunzi wengine.
2. Kujihusisha na ngono, uasherati, ushoga, ulawiti, usagaji na ubakaji.
3. Ulevi wa pombe na kujihusisha na madawa ya kulevya.
4. Kupiga, kupigana au kuchochea ugomvi.
5. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi na kukataa kulipa fidia ya uharibifu.
6. Kukataa kupokea adhabu halali na kuonyesha kiburi,dharau na ufedhuri.
7. **Mwanafunzi kumiliki au kutumia au kukutwa na simu, kifaa chochote au "line" katika mazingira ya Shule.**
8. Kuolewa, kupatikana na ujauzito, kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba.
9. Kushiriki au kushawishi kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu wengine.
10. Kudharau bendera ya Taifa, Viongozi wa Serikali, madhehebu ya dini na viongozi wa shule.
11. Utoro wa muda mrefu, kushindwa kufanya kazi za darasani na nje.
12. Kushindwa kufanya mazoezi/majaribio/mitihani kwa makusudi Pamoja na kutohudhuria maandalizi ya usiku (night preparation).
13. Kutoa lugha ya matusi kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu na viranja.

14. Kulala nje ,kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kutumia vifaa vya umeme kama vile heater,radio na pasi ya umeme.
16. Kutembelea nyumba za walimu/watumishi wa shule bila ya kufuata utaratibu.
17. Kujipikia/kuingiza vyakula bwenini.
18. Kukutwa nje ya shule bila ruhusa na mavazi yasiyoruhusiwa shuleni..
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
20. Kusuka nywele au kunyoa mtindo wa kihuni.

**HITIMISHO MUHIMU**

Tafadhali soma kwa umakini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

1. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile na hakuna mtumishi atakayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi
2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kinatumika na mwanafunzi mmoja tu.
3. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule (Msiba au Ugonjwa) **MUHIMU**
4. Siku ya kuja shuleni kuanza masomo, mwanafunzi aje amevaa sare ya shule (Track Suit)
5. Nguo zote za Kiraia hazitaruhusiwa kabisa kuonekana wala kuvaliwa shuleni.
6. Mzazi/ Mlezi hakikisha mwanao anapimwa afya yake kikamilifu katika Hosptali ya Serikali na si vinginevyo. Ukifanya udanganyifu hatutakubali sababu zozote zitakazotolewa badaye.
7. Hatupokei fedha taslimu shuleni. Hivyo malipo yote yapitie BENKI isipokuwa malipo ya vifaa vinavyoweza kupatikana shuleni.
8. Mwanao haruhusiwi kuja shuleni na kifaa chochote kinachohusiana na umeme kama vile, pasi ya umeme, redio, heater, Charger, computer na **TV. AKIPATIKANA NA VIFAA HIVI ADHABU NI KUONDOLEWA SHULENI**
9. Mwanafunzi kutembelewa shuleni na watu wasio fahamika.
10. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi bwaloni mara kengele ya chakula inapogonga akiwa na vyombo vya chakula.
11. Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalum (special diet) kwa wale wenye matatizo ya kiafya ya kutokula baadhi ya vyakula.
12. Mwanafunzi atumiwe nauli mapema kabla ya kufunga shule ili utaratibu wa usafiri uweze kuandaliwa mapema.
13. Ratiba ya shule huanza saa 11:30 Alfajiri kwa mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na usafi wa mazingira ya bwenini.
14. Mwanafunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kulingana na utaratibu uliowekwa na shule.
15. Mawasiliano ya mwanfunzi na mzazi/mlezi yapitie katika **UONGOZI WA SHULE.**

**VIAMBATISHO MUHIMU**

i. Fomu ya uchunguzi wa Afya (MEDICAL EXAMINATION FORM) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali
ii. Form ya Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Form ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule
iv. Picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
vi. Result slip Original

**Tunakukaribisha sana katika Shule ya Sekondari Robanda**

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

**GEORGE N. CYPRIAN**
**(Mkuu wa Shule)**

**MAHITAJI YA VITABU**

Mzazi/ Mlezi kumbuka kwamba ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Hivyo unaombwa/ unashauriwa na Bodi ya Shule kumnunulia mwanao angalau kitabu kimoja kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma (Vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni)

| Na | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| 1 | BIOLOGY | 1. New understanding Biology for Advanced level. By Suzanne Toole<br>2. Complete Advanced Biology. By Rapacious R<br>3. Biological science By Taylor DJ Adv Manual |
| 2 | CHEMISTRY | 1. A- Level Chemistry by EN RAMSDEN<br>2. A – Level Physical Chemistry 6th Edition by HEYS<br>3. Advanced Chemistry Review by WILLIAM W. Mzumbe book Projects |
| 3 | PHYSICS | 1. Principles of Physics class Xi and Xii by S. CHAND<br>2. A – Level physics by Roger Muncaster |
| 4 | HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI | 1. Historia ya Tanzania na Maadili Shule za Sekondari Kidato cha Tano – TIE 2024 |
| 5 | GEOGRAPHY | An integrated Approach by Waugh D.2009 Geography<br>Landscape Appreciation by Mark night<br>Practical Geography for Africa by KAZIMILI Z 2011 |
| 6 | ACADEMIC COMMUNICATION | 1. Academic Communication For Secondary school - Student Book Form Five – TIE 2024 |

MKUU WA SHULE
ROBANDA SEKONDARI
83 NYAMARA HM
31623 IKOMA SERENGETI

**Kiambatisho A**

## AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI

**i. AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEZO MENGINE.**

Mimi Bw/Bi……………………………………………………Mzazi/Mlezi wa………………………………………………………… (Jina la mwanafunzi) baada ya kusoma maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari Robanda na kuyaelewa vizuri ninaahidi kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo yote yaliyotolewa na kuzingatia waraka wa Elimu namba 5 wa Mwaka 2015 kama mzazi/mlezi nitatekeleza majukumu yote kwa muda mwafuaka ili mtoto aweze kusoma ipasvyo.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi____________________Tarehe______________

Nambaya Simu __________________

**ii. AHADI ZA MWANAFUNZI KUKUBALI KUFUATA MAAGIZO YOTE YA SHULE KAMA MWANAFUNZI.**

Mimi………………………………………………….. baada ya kusoma maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari Robanda na kuyaelewa vizuri ninaahidi kukubaliana na sheria, kanuni, na taratibu zote za shule kwa kipindi chote nitakapokuwa mwanafunzi na kutoshiriki katika migomo, fujo, au makosa ya jinai, nipo tayari kuadhibiwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za shule endapo nitabainika nimekiuka taratibu na sheria za shule.

Sahihi ya mwanafunzi…………………………. Tarehe……………………

***NB.** FOMU HII IKABIDHIWE KWA MAKAMU MKUU WA SHULE SIKU YA KURIPOTI.*



**Kiambatisho B**

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI
## (PERSONAL PARTICULARS FORM)

1. Majina kamili ya mwanafunzi______________________________________
   Jinsi (sex)_______Anwani ya Nyumbani _________
2. Mwaka wa kuzaliwa (Tarehe ____mwezi ___Mwaka______
3. Mahali pa Kuzaliwa Kijiji/ Mtaa____________________Kata____________Tarafa ___________________Wilaya __________________Mkoa_________________
4. Anwani yako ya makazi ya sasa
   Kijiji………………………………………………
   S.L.P……………………………………………
   Mji…………………………………………...
   Shule ya Sekondari Uliyotoka____________________

**JAMAA KATIKA FAMILIA AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU KWA MASUALA YAHUSUYO SHULE**

i. Jina la Baba_____________________
   Namba ya simu ________________
   Kazi yake _____________________
   Anaishi/ Haishi___(**NDIYO/ HAPANA)** *Futa isiyohusika*

ii. Jina la Mama
   Namba ya simu ________________
   Kazi yake _____________________
   Anaishi/ Haishi___(**NDIYO/ HAPANA)** *Futa isiyohusika*

iii. Jina la Mlezi (1) ___________________________________________
   Uhusiano __________________________kazi yake _______________
   Anwani yake ___________________Namba ya Simu _____________

iv. Jina la Mlezi (2) ___________________________________________
   Uhusiano _________________________kaz iyake ________________
   Anwani yake ___________________Namba ya Simu _____________

5. Mimi (Mwanafunzi)___________________________________________ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na Shule hii na ninaahidi kufuata Sheria na Taratibu za Shule kama zilivyotolewa na zitakazotolewa na Uongozi wa Shule.
   Sahihi……………………………………. Tarehe…………………………

***NB.*** ***FOMU HII IKABIDHIWE KWA MAKAMU MKUU WA SHULE SIKU YA KURIPOTI.***




**Kiambatisho C**

# SERENGETI DISTRICT COUNCIL

ROBANDA HIGH SCHOOL,
P.O. BOX 77,
83 NYAMARA HM
**31623 IKOMA – SERENGETI**
05.05.2026

**FOR MEDICAL EXAMINATION**

This form must be completed by a government medical officer
Student full name…………………………………………………………………………
Present age…………………………………………………………………..……
Blood test……………………………………………………………….………………
Stool examination…………………………………………………..………………..
Tb test……………………………………………………………………...………………
Asthma…………………………………………………………………………………..…
Eyes disorder ………………………………………………………………………………
Anemia………………………..……………………………………………………..
Chest………………………………………………………………………………………
Operation…………………………………..…………………………………………
Serious accident…………………………...……………………………………………
Any other infection disease…………………………………………………………
Pregnancy………………………………………........(in case of a girl student)

**ADDITIONAL INFORMATION**

E.g. physical defect of impartment, chronic family disease……………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

I certify that I have personally examined (name of a student) ………………………………………………… and found his/her fit/unfit pursue further studies.

Signature…………………Designation…………………………………
Official stamp

Station …………………………………… Date………………………

N.B This form has to submitted to the Second Master immediately you report at School

# MAVAZI YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO



**GAUNI LA KUSHINDIA**



**SKETI YA KUSHINDIA**



**T-SHIRT**



**SKETI YA DARASANI**



**SWETA LA DARASANI**